MAISHA YA MKRISTO SOMO LA 1
TUMAINI NI ZAWADI YA THAMANI SANA
KATIKA MAISHA YAKO.
TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUANGALIA VIFUNGU VYOTE REJEA.

Tumaini ni kati ya zawadi (Vipawa) vya thamani sana kutoka kwa Mungu.

Mungu kwa upendo wake kwetu, alifahamu sana kwamba watu watahitaji alipokuwa akishughulikia utu wetu; yeye amefanya iwezekane kwetu kuitegemea hata kama mazingira yangekuwa ya hatari sana. Hebu fungua Biblia yako na usome Waraka wa pili wa Mtume Paulo kwa Wathesalonike sura ya 2 mistari ya 16 na 17.

Mwanzo kabisa wa sura za kitabu cha Biblia; tunaweza kufahamu watu walioishi maisha ya matumaini kuna uhusiano sana kati ya Tumaini na Imani na tutaangalia Imani katika somo la 11.

Katika Waraka kwa Waebrania sura ya 11 mstari wa 1 tunasoma kwamba Imani ni kuwa na uhakika na mambo yatarajiwayo. Tunapotarajia ufahamu wetu unakuwa na picha za mambo tunayoyatazamia katika akili zetu, mambo yale tunayoyapenda kuyafanya kwa sababu sisi ni Wanadamu, kwa mambo yale tunayopenda yawe yetu.

Tumaini ni kati ya mambo matatu ambayo Mtume Paulo aliyaona kuwa ndiyo hasa tabia ya kweli ya mwanafunzi wa Kristo. Imani, Tumaini na Upendo.

Kwa sababu hiyo hebu tuwaangalie baadhi ya watu katika Biblia waliokuwa na tumaini na wachache ambao hawakuwa na tumaini.

Tutaanza kwa kumwangalia Yesu Kristo kwa kuangalia maneno ya Mtume Petro aliyekuwa wa kwanza kati ya wanafunzi wake. Maneno hayo yanapatikana katika Matendo ya Mitume sura ya 2 mstari wa 26. Petro alikuwa akisema kuhusu Yesu lakini akitumia maneno ya Mfalme Daudi kutoka Zaburi 16 mstari wa 9. Kama wewe mwenyewe ndiye ungechukua nafasi ya YESU wakati alipokubali kwa hiari yake kukamatwa, na kuteswa na hatimaye kufa msalabani, utakubali ni kwa jinsi gani Unabii uliotabiriwa na Daudi katika Zaburi hii ulivyokuwa wa muhimu kuhusu Yesu.

Kisha tutaangalia maneno machache ya Nabii Yeremia aliyeteseka mara nyingi kwa kuogopa kunena ujumbe wa MUNGU kwa watu wa Yerusalem. Aliwaeleza wao pamoja na Wafalme wao kwamba ili waishi ni lazima wajisalimishe kwa jeshi la Baberi. Hapo Yeremia aliteswa kama msaliti hadi kutupwa katika shimo lenye kina kirefu sana cha Jiji la Yerusalem. Soma Yeremia sura ya 38, sura ya 6 na usome habari hii. Katika maombolezo Yeremia anaelezea huzuni yake na mateso yake. Angalia maombolezo sura ya 3 mstari wa 1 na 6.

Somo hili ni muhimu sana kwetu kwa kuwa katika mateso na hatari bado Yeremia aliweza kuyaona mambo yakienda sawa sawa. Katika mstari wa 18, tunaweza kujaribiwa namna hiyo katika siku za shida katika maisha yetu lakini hasa soma mistari ya 19 na 21.

Yeremia mara akakubali kuwa alikuwa angali hai na maneno ya ajabu kwetu ya kukumbuka yanapatikana mistari ya 24 hadi 26.

Kwa sababu hiyo Tumaini ni kusubiri jambo, tunatakiwa kungoja Wokovu kutoka kwa Mungu.

Habari nyingi zimeandikwa kuhusu kurudi Yesu Kristo hapa duniani kuwa Mfalme. Tungependa itokee leo hii, maana kuna matatizo mengi sana hapa duniani ambayo yangeisha kabisa. Wanadamu ingawaje wamejitahidi kwa bidii zao lakini hata hivyo wameshindwa. Maneno ya Nabii Yeremia ni muhimu kwetu leo kuyakumbuka. Tuendelee kusubiri kwa saburi saa MUNGU aliyoiweka.
Na sasa tufikirie mfano wa Abrahamu aliyeacha nyumba yake na vyote alivyokuwa navyo akifuata maono ya wakati ujao. Wakati Mungu alipomuahidi mambo ambayo yangetokea wakati ujao mbali, ni dhahiri kwamba Abrahamu angehitaji mtoto wa kuendelea baada yake na yamkini wajukuu na vijukuu! Abrahamu alikuwa na miaka 75 alipohamia Hanani na alikuwa na miaka 100, Isaka alipozaliwa Miaka 25, muda mrefu sana kusubiri kwa imani.
Inatisha sana kuishi maisha ya bila ya matumaini kwa muda kidogo tu, Ayubu alikuwa katika hali hii Ayubu sura ya 7 mstari wa 3 hadi 7. Unaposoma matatizo yote yaliyompata yeye na familia yake ni rahisi sana kuelewa ni kwa nini alifikiria hivyo. Hata hivyo baada ya kupingana na ushauri wa rafiki zake aliyatarajia maisha yaliyoboreshwa na katika sura ya 19 licha ya maisha yake kuwa mabaya sana ikiwa ni pamoja na ugonjwa uliomsumbua ghafla alibadilisha kilio chake (maombolezo) na akanena mambo tunayoamini siku hizi kuhusu KIFO na Ufufuo. Tunapaswa kushangazwa na maono yake yaliyo halisi kuhusu wakati ujao na tumaini lake thabiti la milele kuwa yalikuwa kiini cha pekee katika nafsi yake.

Soma mistari ya 25 hadi 27. " Nina mjua Mkombozi wangu yu hai". Haya ni maneno mazuri ya kuzingatia hasa tunapokuwa katika mateso na hata kuwa na dhiki katika maisha. Kwa hiyo tumaini ni muhimu sana kuwa nayo, tumaini katika ahadi zote za Mungu Baba kuwa zitatimia hapa duniani. Kwa kuwa maisha ya watu yataweza kuboreshwa. Bado njia nzuri ya kuweza kulielewa neno hili tumaini.

Mitume wa Yesu walilitaja kuwa ni TUMAINI PEKEE, ilikuwa njia ya kuelezea imani kuhusu YESU na ufalme wake ujao, maneno waliyoyatumia ni:
"Tumaini la uzima wa milele" Tito sura ya 3 mstari wa 7
"Tumaini la wokovu" Waraka wa kwanza kwa Wathesalonike sura ya 5 mstari wa 8 .
"Tumaini la Utukufu" Wakolosai sura ya 1 mstari wa 27.

Mtume Paulo aliandika katika Waraka kwa Warumi sura ya 4 mstari wa 18 kuwa - tumeokolewa kwa njia ya Imani na katika waraka wa kwanza kwa Wakorinto Sura ya 15 mstari wa 19 anatuhimiza ili tunyamaze na kufikiri. 'Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote". Kuwa na tumaini kwa Wanasiasa, mabalozi (wanadiplomasia), maaskari, hata mashirika yanayojitolea sana kwa misaada ya kiutu kama vile Medecin Sans frontiers, Save the children (Okoa watoto), Oxfam na msalaba mwekundu kuwa yanaweza kubadili dunia [ulimwengu] kuwa mahali / sehemu nzuri ya kudumu ni dhahiri kuwa tutavunjika mioyo.

Paulo anasema inakuwa tofauti kabisa wakati unapo tumaini katika Yesu kwa sababu amefufuka kutoka kaburini, yu hai, na atarudi tena duniani.

Wakati Yesu atakaporudi kusimamisha ufalme wake, wanafunzi wake wote wa nyakati zote za historia (watafufuka) wataamka toka makaburini na ikiwa walitunza imani yao, watapewa uzima udumuo milele katika dunia ya kupendeza na ya amani.

Bwana Yesu Kristo atakuwa Mfalme wa watu wote na atatawala kwa nguvu za Mungu, Kwa haki pamoja na hekima na upendo.

Ubatizo katika jina la Yesu ni njia inayofungulia mambo haya mazuri sana. Mtume Petro aliandika katika waraka wake wa kwanza sura ya 1 mstari wa 3.

Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu".

Ubatizo ni kuzaliwa mara ya pili kwa ajili ya uzima mpya kama mwanafunzi wa Yesu.

Tunapaswa kushirikisha wengine tumaini hili la uzima ambalo ni jema na linalo tosheleza katika maisha yetu.

* Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu. 1Petro 3:15

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)